AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA

**Addis Ababa, Ethiopia S.L.P 3243 Simu: +251 115 517 700 Nukushi: +251 115 517 844**
**Tovutu:** www.au.int

**BARAZA KUU**
**Mkuatano wa Arobaini na nne wa Kawaida**
**Tarehe 15 Januari - 15 Februari 2024**
**Addis Ababa, ETHIOPIA**

**EX.CL/1504(XLIV)**
Matini chanzi: Kiingereza

# TAMKO LA DAR-ES- SALAAM KUHUSU MKUTANO MKUU WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU RASILIMALI WATU BARANI AFRIKA MNAMO 2023

***(Kipengele kilichopendekezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)***

# ANDIKO DHANA KUHUSU AJENDA ILIYOPENDEKEZWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUHUSU MKUTANO WA RASILIMALI WATU BARANI AFRIKA 2023.

**USULI**:
1. Afrika iliingia katika muongo uliopita ikiwa na upungufu mkubwa wa rasilimali watu, ikiwa na wastani wa chini kabisa wa Kielezo cha Rasilimali watu (HCI) ikilinganishwa na maeneo mengine. Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazoingiliana ambazo zinahatarisha rasilimali watu: kupanda kwa mfumuko wa bei na viwango vya riba, ukosefu wa ajira, na kupunguzwa kwa misaada ya maendeleo; wakati huo huo, mgogoro wa Ukraine umesababisha kupanda kwa mfumuko wa bei. Pamoja na hayo, kanda hii inakabiliwa na changamoto ya viwango vya juu vya ukuaji wa idadi ya watu ambavyo vinasababisha vikwazo vikubwa vya kifedha katika kutoa huduma za msingi, uhaba mkubwa wa ajira na kiwango kidogo cha mlimbikizo wa rasilimali watu.

2. **Hata hivyo, ongezeko la idadi ya watu** pia ni miongoni mwa rasilimali kuu za Afrika-watu wake. Ifikapo mwaka 2050, eneo hilo linatarajiwa kuwa limeongeza idadi ya watu mara mbili hadi bilioni 2.2. Tofauti na mienendo duniani kote, idadi ya watu wa Katika Nchi za Kusini (SSA) itaendelea kukua zaidi baada ya mwaka 2100. Idadi ya watu walio katika umri wa kufanya kazi itafikia watu bilioni 1.5 ifikapo 2075 wakati ile ya watoto wenye umri wa miaka 0-14 itafikia milioni 700 ifikapo 2075. Uwekezaji wa wakati katika elimu na hali ya afya ya wakazi wake, pamoja na uundaji wa nafasi za kazi kunaweza kufungua uwezo mkubwa wa ukuaji wa uchumi wa demografia hizi na kunufaika na idadi hiyo ya watu. Kuchukua hatua za haraka katika kujenga rasilimali watu—maarifa, ujuzi, na afya ambayo watu hukusanya katika maisha yao—ni kipaumbele cha dharura cha kiuchumi.

3. **Mfumo wa sasa wa elimu umefikia kikomo chake**, na mahitaji yanazidi tu kuongezeka. Kufikia 2050, Afrika itawakilisha zaidi ya 40% ya watu wenye umri wa kwenda shule (miaka 0-14) katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Mara tu mwaka 2023, Afrika itaipita Asia Kusini, na kufikia mwaka 2060, karibu watoto milioni 750 wanatarajiwa kuwa katika mfumo wa elimu. Umaskini wa kujifunza unaotokana na UVIKO-19 unatarajiwa kuongezeka hadi 89%, huku wale walio na shida kubwa ya kusoma wakibaki nyuma zaidi. Kabla ya janga hili, mtoto wa kawaida katika eneo hilo angeweza kutarajia kumaliza miaka 5 tu ya masomo ya shule na umri wa miaka 18.

4. **Ujenzi wa mifumo ya afya** umechukua nafasi ya pili, ikizingatiwa kutilia mkazo mapambano dhidi ya janga hili na kusababisha kuongezeka kwa magonjwa ambayo yalikuwa yametokomezwa. Mbali na milioni 4.4 ambao hawajapata chanjo yoyote, kuna visa vya kutokamilika kwa chanjo, huku 25% ya watoto wamepata dozi 1 tu kati ya 3 zinazohitajika kwa DPT. Mnamo 2020, nchi 10 bora zilizo na visa vingi vya saratani ya shingo ya kizazi zote zilikuwa barani Afrika.

5. **Kuhusiana na ajenda hii**, jinsia ni mada mtambuka ambayo ni moja ya misingi muhimu ya kufikia matokeo ya Rasilimali watu. Uwekezaji kwa wanawake, watoto na

vijana ili kuhakikisha matunzo sawa na nafuu yana uwezekano wa kuleta mabadiliko ya kufungua fursa za maisha, kusaidia ukuaji jumuishi na kuendeleza haki zao. Kanda ya Afrika inakabiliwa na tofauti kubwa za kijinsia. Miongoni mwa Watoto Walio nje ya Shule, kuna wanaume milioni 45.5 na wanawake milioni 52 wa janga la awali. Kwa upande mwingine, unyanyasaji wa kijinsia (GBV) na uzazi wa mapema ni miongoni mwa vikwazo vikuu vinavyozuia wasichana kuhudhuria shule na kustawi, na kuathiri karibu 30% ya wasichana katika kanda hiyo. Nchi ambazo zilionyesha utayari wa kudumu kwa uwekezaji wa kifedha na kimfumo unaohitajika ili kuboresha ustawi wa wanawake, watoto, na vijana zilidumisha mifumo thabiti ya afya na matokeo bora.

**6. Kutokana na hali hiyo**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia kwa pamoja waliandaa Mkutano wa Wakuu wa Nchi kuhusu Rasilimali Watu barani Afrika chini ya kaulimbiu "Kuharakisha Ukuaji wa Uchumi wa Afrika: Kukuza Tija kwa Vijana kwa Kushughulikia Malengo ya Mafunzo na Ujuzi", jijini Dar es Salaam. Tarehe 25 hadi 26 Julai, 2023. Mkutano huo ambao uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhudhuriwa na nchi 44 za Afrika pamoja na taasisi za kikanda na kimataifa ikiwemo Kamisheni ya Umoja wa Afrika, vipaumbele vya sera, changamoto, malengo muhimu, na kuwa tayari kuwekeza kwa watu, hasa katika kujifunza, ujuzi, afya na uvumbuzi ili kunufaika kikamilifu na idadi ya watu barani Afrika.

7. **Baada ya kuhitimisha Mkutano huo**, Wakuu wa Nchi na Serikali walipitisha Azimio la Dar es Salaam, ambalo pamoja na mengine, linampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu nchi na Serikali kuhusu Rasilimali Watu Afrika. Pia inajitolea kutekeleza Ajenda ya Umoja wa Afrika, kwa msisitizo mpya wa kunufaika na idadi ya watu kwa kuzingatia elimu, kazi na ajira zenye heshima, usalama wa kijamii na ulinzi, afya na lishe, pamoja na uwezeshaji wa vijana. Aidha, Mkutano huo umeazimia kuongeza upatikanaji, uwezo wa kumudu na kuhakikisha elimu bora pamoja na kupunguza umaskini wa kujifunza barani Afrika kwa angalau robo mwaka 2030 na kuboresha idadi ya watu wanaojua kusoma na kuandika kufikia asilimia 75 ifikapo mwaka 2030. Aidha, Wakuu wa Nchi na Serikali kuwa tayari kutoa mafunzo ya ujuzi kwa nyongeza ya milioni 19 ili kupata ujuzi wa kidijitali wa kazi ifikapo 2030 na kulenga Uwiano wa Jumla wa Uandikishaji wa elimu ya juu wa 20%. Hatimaye, Mkutano huo unaahidi kuongeza rasilimali za ndani ili kufikia matokeo ya rasilimali watu kwa 3% ifikapo 2030.

8. Kwa hiyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawasilisha Rasimu ya Azimio lifuatalo kwa ajili ya kuzingatiwa na Mkutano Mkuu:

(1) **Unarejelea** kauli mbiu ya Umoja wa Afrika kwa mwaka wa 2024, ambayo ni kuhusu Elimisha Mwafrika kwa Karne ya 21: Kujenga mifumo thabiti ya elimu kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa mafunzo jumuishi, ya kudumu, bora na yanayofaa barani Afrika.

(2) **Unapokea** changamoto za Rasilimali Watu zinazolikabili bara laAfrika;

(3) **Unampongeza** Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Rasilimali Watu wa Afrika uliofanyika Dar es Salaam, Tanzania, kuanzia tarehe 25 hadi 26 Julai, 2023;

(4) **Unaridhia Tamko** la Mkutano Mkuu wa Dar es Salaam kuhusu Rasilimali Watu ;

(5) **Unahimiza** Nchi Wanachama kutekeleza vipengele muhimu vya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Rasilimali Watu barani Afrika, ikijumuisha dhamira ya kuongeza rasilimali za ndani kuelekea matokeo ya rasilimal watu kwa 3% ifikapo 2030 ; na

(6) **Unatoa Wito kwa** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Shirika la Maendeleo la NEPAD, Benki ya Dunia na washirika wengine kuongeza msaada kwa nchi wanachama katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya rasilimali watu kwa angalau 5% ifikapo 2030.




# TAMKO LA DAR ES SALAAM

## MKUTANO MKUU WA

## WAKUU WA NCHI NA SERIKALI BARANI AFRIKA KUHUSU RASILIMALI WATU, TAREHE 26 JULAI 2023

**Kuwekeza kwa Watu kwa ajili ya Kujenga Uchumi wenye tija ya Juu, Jumuishi na Ustahimilivu**

## UTANGULIZI

**1. Sisi, Wakuu wa Nchi na Serikali za nchi wanachama wa Umoja wa Afrika unaosimamiwa na** Serikali ya Tanzania, tulikutana Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Julai 2023 kwa ajili ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa Rasilimali Watu**.**

**2. Tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia jambo hili na kuandaa mkutano huu muhimu wa kujadili vipaumbele vya sera, changamoto, malengo muhimu na ahadi za kuwekeza kwa wananchi wetu hususan katika kujifunza, ujuzi, afya, na uvumbuzi ili kunufaika kikamilifu na idadi ya watu wa mataifa yetu.

**3. Tunatambua na kuthamini uungaji mkono** wa Benki ya Dunia na washirika wengine wa maendeleo wa nchi zetu katika utekelezaji wa Ajenda 2063: Afrika Tunayoitaka na Ajenda 2030 kuhusu Maendeleo Endelevu, ili kuboresha ustawi wa watu wetu.

**4. Tunakaribisha mtindo wa mahusiano wa Kundi la Benki ya Dunia** kwa kukuza moyo wa ushirikiano unaodhihirishwa kwa kuelewa na kubadilishana uzoefu kuhusu changamoto ili kuzisaidia vyema serikali katika utekelezaji wa mikakati yao ya kitaifa, kupitia vyombo vya ufadhili vilivyorekebishwa kulingana na mahitaji yao, kama inavyoonyeshwa kupitia mpango wa Abidjan. Pia tunatambua jukumu muhimu la ushirikiano uliopo katika kusaidia nchi ili kuchochea ufadhili zaidi kwa matokeo ya rasilimali watu ili kuimarisha zaidi ushirikiano.

**5. Tunapokea kwa masikitiko** athari mbaya zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa, janga la Uviko-19, na vita vya Urusi na Ukraine dhidi ya ukuzaji wa rasilimali watu, haswa katika nchi za Kiafrika**.**

**6. Tunatambua na kushukuru** juhudi zinazofanywa na serikali nyingi za Afrika katika kuboresha hali ya maendeleo ya binadamu, ikiwa ni pamoja na kuongeza mgao wa bajeti ya kitaifa kwenye elimu, afya, usalama wa chakula na lishe**.**

**7. Tunakubali kuzingatia "Tamko la Dar es Salaam kuhusu Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa Rasilimali Watu"** katika kutoa kipaumbele kwenye afua za serikali na washirika wa maendeleo katika miaka ijayo kuhusu Maendeleo ya Rasilimali Watu.

**VIPAUMBELE VYA UWEKEZAJI KATIKA RASILIMALI WATU**

**Kutambua** kwamba vipaumbele vya kuwekeza na kulinda rasilimali watu vitakuwa muhimu katika kujenga upya uchumi wenye tija ya juu, jumuishi na thabiti zaidi.

**8. Unathibitisha,** kwamba mtaji wa watu unajumuisha pamoja na mambo mengine mali kama vile elimu, ujuzi, afya, lishe, maji safi na salama na usawa wa kijinsia ambayo ni

muhimu kwa maendeleo katika nchi za Afrika na kuchukua jukumu muhimu katika mabadiliko ya uchumi wa Afrika**.**

**9. Unakiri kwamba uwekezaji** kwa watu ni muhimu kwa ajili ya kujenga ukuaji endelevu, ustahimilivu, na shirikishi barani Afrika, na kwamba uwekezaji katika rasilimali watu kwa ajili ya matokeo bora ya kijamii na kiuchumi katika siku zijazo kupitia elimu bora, ujuzi na kazi, huduma za afya na lishe ni muhimu katika kukomesha umaskini uliokithiri na kuunda jamii shirikishi zaidi**.**

**10. Unatambua kwamba** Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ina alama za chini zaidi kuliko kanda zote za dunia kwenye Kielezo cha Rasilimali watu cha Benki ya Dunia, kipimo ambacho kinabainisha mchango wa afya na elimu kwa tija ya kizazi kijacho cha wafanyakazi.

**11. Unatambua zaidi,** kwamba ingawa kuna matokeo bora ya upatikanaji wa huduma za afya kwa kaya, uandikishaji shule, vistawishi na zana za kuboresha maisha - lengo la rasilimali watu na ubora wa maisha bado liko nyuma kwa kiasi kikubwa, hasa katika muktadha wa migogoro mingi inayoikabili dunia.

**12. Unafahamu kwamba** kuendeleza rasilimali watu barani Afrika kunahitaji mipango na ufadhili mkubwa ulioratibiwa pamoja na juhudi madhubuti za kuimarisha wingi, ufanisi na athari za uwekezaji kwa watu.

**13. Unazingatia hitaji** la dharura la kushughulikia mageuzi ya sera ya maendeleo na ubunifu wa kitaasisi kwa kutilia mkazo utekelezaji thabiti zaidi, ambao utawawezesha vijana wa Afrika kukua wakiwa na afya bora na wakiwa na maarifa, ujuzi na umahiri sahihi wa kushindana katika ulimwengu wa uchumi wa kidijitali**.**

**14. Hivyo, kubainisha haja ya** kuongeza fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya utekelezaji ya kikanda na nchi na mafunzo ya nchi mbalimbali**.**

**15. Unatambua umuhimu** wa kushughulikia matatizo yanayohusiana na maendeleo ya rasilimali watu ili kuboresha uwezo wa bara la Afrika, kushughulikia changamoto za maendeleo ya rasilimali watu na kutumia fursa zinazojitokeza.

**Ili kufanya hivyo, sisi:**

**16. Tupo tayari** kutekeleza Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika, kwa msisitizo mpya wa kutumia Idadi ya Watu kwa manufaa  kwa kuzingatia Elimu, Kazi na Ajira zenye Staha, Usalama na Ulinzi wa Jamii, Afya na Lishe, pamoja na uwezeshaji wa Wanawake na Vijana.

**17. Hasa, tunaahidi:**

**a) Kutoa kipaumbele kwenye Elimu na Ukuzaji Ujuzi:** Kwa kutambua kwamba elimu bora na ukuzaji wa ujuzi ni msingi muhimu kwa maendeleo ya rasilimali watu, tupo tayari kuongeza uwekezaji katika mifumo ya elimu, kuanzia elimu ya chekechea hadi mafunzo ya elimu ya juu na ufundi stadi, ili kuhakikisha upatikanaji sawa na matokeo bora ya kujifunza. Tutatoa kipaumbele kwenye ukuzaji wa ujuzi wa kimsingi na ujuzi unaofaa kwa siku zijazo za kazi, ujasiriamali, na uvumbuzi, kukuza utamaduni wa kujifunza maisha yote. Hivyo, tupo tayari kuongeza upatikanaji, uwezo wa kumudu na kuhakikisha elimu bora na pia kupunguza umaskini wa kujifunza katika nchi zetu kwa angalau robo ifikapo mwaka 2030 na kuongeza idadi ya watu wanaojua kusoma na kuandika kufikia 75% ifikapo 2030.

**b) Kuimarisha Afya na Ustawi:** Tunaahidi kuwekeza katika mifumo inayofikiwa, nafuu, na yenye ubora wa huduma za afya, tukizingatia maisha ya mtoto, huduma ya afya ya kinga, huduma za afya ya msingi, na kupunguza vifo vya uzazi, watoto wachanga, na watoto. Tutashughulikia mzigo wa magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyo ya kuambukiza, na masuala ya afya, kukuza ustawi wa jumla kwa Waafrika wote. Kuhusu lishe, tupo tayari kupunguza upotevu, kudumaa na watu wenye uzito pungufu. Tupo tayari kwa nchi zetu kufikia chanjo ya 90% ifikapo 2030. Pia tupo tayari kupunguza

uzazi hadi 70 kwa kila watoto 100,000 wanaojifungua na vifo vya watoto chini ya miaka 5 hadi 25 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai na kudumaa kwa 40% katika nchi zetu ifikapo 2030.

**c) Kuwawezesha Wanawake na Wasichana**: Tunasisitiza umuhimu wa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana katika maendeleo ya rasilimali watu. Tupo tayari kuondoa vikwazo vinavyozuia wanawake na wasichana kupata elimu, huduma za afya na fursa za kiuchumi. Tutakuza sera na mipango inayosaidia ujumuishaji wa jinsia, ukuzaji wa uongozi, na ujasiriamali kwa wanawake na wasichana. Tupo tayari kuongeza upatikanaji wa elimu ya sekondari na elimu ya juu kwa angalau wasichana milioni 20 wa ziada katika bara la Afrika ifikapo 2030, ili kufikia 40% ya wasichana wenye umri wa miaka 15 kupokea dozi zinazopendekezwa za chanjo ya HPV ifikapo 2025, na kupunguza mimba za utotoni kwa nusu ifikapo 2030.

**d) Kukuza Uundaji wa Ajira na Fursa za Kiuchumi**: Tunaelewa haja ya kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kubuni nafasi za kazi na fursa za kiuchumi. Tupo tayari kutekeleza sera zinazovutia uwekezaji wa ndani na nje, kukuza ujasiriamali, na kuwezesha ukuaji wa biashara ndogo na za kati. Tutazipa kipaumbele sekta zenye uwezekano mkubwa wa kuzalisha nafasi za kazi, kama vile kilimo, nishati mbadala, teknolojia ya kidijitali na utengenezaji. Tupo tayari kutoa mafunzo kuhusu ujuzi kwa nyongeza ya milioni 19 ili kupata ujuzi wa kidijitali wa kazi ifikapo 2030 na tunalenga Uwiano wa Jumla wa Uandikishaji wa elimu ya juu wa 20%.

**e) Kuhakikisha Ulinzi na Ushirikishwaji wa Kijamii**: Tunasisitiza umuhimu wa mifumo ya ulinzi wa kijamii ili kulinda idadi ya watu walio hatarini zaidi. Tupo tayari kutengeneza mifumo kamili vya usalama wa kijamii, ikijumuisha bima ya kijamii, upatikanaji wa nyumba bora, maji safi, usafi wa mazingira, na umeme. Tutaweka kipaumbele cha kujumuisha watu wenye ulemavu, wakimbizi, na watu waliokimbia makazi yao ndani ya nchi, kuhakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma. Kuhusiana na hili, tunaahidi

kwamba nchi zote katika bara hili zitakuwa na mfumo kamili wa uendeshaji wa kijamii ifikapo 2030.

**f) Kuimarisha Utafiti na Ubunifu**: Tunatambua jukumu la utafiti na uvumbuzi katika kuendeleza maendeleo ya rasilimali watu. Tutaweka mazingira wezeshi kwaajili ya utafiti wa kisayansi, uhamishaji wa teknolojia na uvumbuzi, tukihimiza ushirikiano kati ya wanazuoni, viwanda na serikali. Tutawekeza katika miundombinu ya utafiti na maendeleo na kukuza ujasiriamali na mifumo ya uvumbuzi ili kuendeleza ukuaji endelevu na uundaji wa nafasi za kazi.

**g) Kuhamasisha Rasilimali na Mashirikiano**: Tupo tayari kuhamasisha rasilimali za ndani, kuongeza uwekezaji wa serikali na wa kibinafsi, na kutumia msaada wa kimataifa. Tutaimarisha ushirikiano kati ya serikali, mashirika ya kimataifa, mashirika ya kiraia, sekta ya kibinafsi, na wanazuoni ili kuendesha hatua zilizoratibiwa na kubadilishana maarifa. Tupo tayari kuongeza rasilimali zetu za ndani ili kufikia malengo ya Rasilimali Watu kwa asilimia 3 ifikapo 2030.

**18. Na kwa ajili ya lengo hili, sisi:**

**a) Tunasisitiza wito** wa kuongeza misaada kwa bara la Afrika ili kujijenga upya vyema zaidi baada ya janga lililotokana la UVIKO-19 na majanga mengine mengi.

b) **Tunatambua** jukumu la washirika wa maendeleo baina ya nchi na nchi nyingi, pamoja na sekta binafsi, asasi za kiraia, taasisi za ushauri wa kitaalam na wasomi wanaohusika katika Kuwekeza kwa Watu wetu na kuwataka kujitahidi kuoanisha msaada wowote na mipango ya maendeleo ya taifa na mikakati ya rasilimali watu. Kwa muktadha huu, tunatoa wito kwa washirika wa maendeleo kuongeza ufadhili na misaada ya kiufundi kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya Rasilimali Watu kwa 5% ifikapo 2030.

**19. Kwa lengo la kupata mustakabali ulio imara na wenye mafanikio kwa watoto wetu na kizazi kijacho**, tunakubali tamko hili na kuinua mikono yetu kwa mshikamano na washirika wetu wa maendeleo ili kujenga eneo lenye watu wenye afya njema ambapo wasichana na wavulana wote wanafika shuleni tayari kujifunza, wajifunze kweli ndani na nje ya darasa, wapate ujuzi unaofaa na waingie kwenye soko la ajira kama wananchi wenye tija na walioridhika.

**ORODHA YA NCHI ZINAZOSHIRIKI**

1. Algeria
2. Angola
3. Benin
4. Botswana
5. Jamhuri ya Burundi
6. Cameroon
7. Cabo Verde
8. Jamhuri ya Afrika ya Kati
9. Comoros
10. Côte d'Ivoire
11. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo
12. Djibouti
13. Misri
14. Equtorial Guinea
15. Eswatini
16. Ethiopia
17. Gambia
18. Gabon
19. Ghana
20. Kenya
21. Liberia
22. Libya
23. Malawi
24. Madagascar
25. Mauritania
26. Mauritius
27. Msumbiji
28. Namibia
29. Nigeria
30. Rwanda
31. Sao Tome and Principe
32. Senegal
33. Ushelisheli
34. Sierra Leone
35. Somalia
36. Jahuri ya Afrika Kusini
37. Jamhuri ya Sudan Kusini
38. Tanzania
39. Togo
40. Tunisia
41. Uganda
42. Saharawi
43. Zambia
44. Zimbabwe

**AFRICAN UNION UNION AFRICAINE**

**African Union Common Repository** **http://archives.au.int**

Organs Council of Ministers & Executive Council Collection

2024-01-15

# Dar-Es- Salaam Declaration on Africa Human Capital Heads of State 2023 Summit (Item proposed by the United Republic of Tanzania)

African Union

African Union

https://archives.au.int/handle/123456789/10556

*Downloaded from African Union Common Repository*